

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA KWA KADA ZA AFYA NA UALIMU

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) imepata kibali cha ajira za Watumishi wa Kada mbalimbali za Afya **2,726** kwa ajili ya Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na **Walimu 6,949** wa Shule za Msingi na Sekondari watakaofanya kazi chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

Kwa sababu hiyo, wahitimu kutoka kwenye Vyuo vya Elimu ya Juu, Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Afya vinavyotambuliwa na Serikali wanatangaziwa kutuma maombi yao ya nafasi za kazi kuanzia tarehe **09 - 23 Mei, 2021**. Nafasi za ajira zilizopo ni kwa wahitimu wa Astashahada (Certificate), Stashahada (Diploma) na Shahada (Degree).

A: TARATIBU ZA KUOMBA AJIRA ZA UALIMU

Walimu wote wenye sifa watume maombi kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha **ajira.tamisemi.go.tz** kwa utaratibu ufuatao: -

- i. Walimu wote wenye sifa ambao hawakuomba ajira za ualimu (tarehe 07.09.2021) watume maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha **ajira.tamisemi.go.tz**,
- ii. Walimu walioomba ajira kwa njia ya mtandao kufuatia Tangazo la Ajira la tarehe 07 Septemba, 2020, wanaelekezwa kuingia kwenye *akaunti* zao walizotumia wakati wa kutuma maombi ili kuhakiki usahihi wa taarifa na viambatisho walivyotuma hapo awali; na

- iii. Tangazo hili linawahusu wahitimu wa Kozi za Ualimu kuanzia mwaka 2012 hadi mwaka 2019.

2.0 SIFA ZA WAOMBAJI

2.1 SIFA ZA KITAALUMA ZA MWOMBAJI

Walimu wanaotakiwa kutuma maombi wawe na Sifa za kitaaluma kama ifuatavyo:

2.1.1 WALIMU WA SHULE ZA MSINGI

Walimu wanaoomba kuajiriwa kufundisha Shule za Msingi wawe na Sifa zifuatazo:

- i. **Mwalimu Daraja la IIIA:** Mhitimu wa Astashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, Astashahada ya Ualimu Elimu ya Michezo, Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali na Astashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum;
- ii. **Mwalimu Daraja la IIIB:** Mhitimu wa Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Awali, Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Msingi na Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum; na
- iii. **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Shahada ya Ualimu katika masomo ya “English Language, History na Geography”.

2.1.2 WALIMU WA SHULE ZA SEKONDARI

- i. **Mwalimu Daraja la IIIB:** Mhitimu wa Stashahada ya Ualimu wa Masomo ya “Physics, Mathematics, Biology na Chemistry”;
- ii. **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Shahada ya Ualimu aliyesomea Elimu Maalum kwa Masomo ya “Physics, Chemistry, Biology na Mathematics”;
- iii. **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Shahada ya Ualimu wa Masomo ya “Physics, Mathematics, Chemistry na Biology”;
- iv. **Mwalimu Daraja la IIIC:** Mhitimu wa Stashahada ya Uzamili katika Elimu (Post Graduate Diploma in Education) lazima awe mwenye Shahada ya Kwanza (Bachelor Degree) yenye Masomo yaliyotajwa katika (ii) na (iii) hapo juu.

2.2. WAHITIMU WALIOSOMA NJE YA NCHI

- i. Waombaji wote waliosoma Elimu ya Sekondari nje ya nchi wanatakiwa kupata Namba ya Ulinganifu wa Matokeo (Equivalent Number) inayoanza na Herufi **EQ...** kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania ili kuwawezesha kuingia kwenye Mfumo wa Ajira; na
- ii. Waombaji waliosoma Vyuo Nje ya Nchi wanatakiwa kupata Ithibati ya masomo yao kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ili vyeti vyao viweze kutambuliwa na kupata uhalali wa kutumika hapa nchini.

3.0 SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI WA AJIRA ZA UALIMU

Mwombaji wa nafasi zilizoainishwa hapo juu awe na sifa za jumla zifuatazo: -

- i. Awe ni Mtanzania;
- ii. Awe na umri usiozidi miaka arobaini na tano (45);
- iii. Awe hajawahi kufukuzwa, kuacha kazi au kustaafishwa katika Utumishi wa Umma;
- iv. Awe na namba ya kitambulisho cha Taifa;
- v. Waombaji wenye Shahada na Stashahada za NACTE na TCU (UDOM) waambatishe Cheti cha Kuhitimu Mafunzo na “Transcript”. Waombaji wa Astashahada na Stashahada za NECTA waambatishe Cheti cha Mafunzo katika sehemu mbili (weka cheti na weka “transcript”);
- vi. Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne na Sita;
- vii. Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa; na
- viii. Maelezo Binafsi (CV), yakionesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani.

B: TARATIBU ZA KUOMBA AJIRA KADA ZA AFYA

Wataalamu wa Kada za Afya wenye sifa watume maombi kwa njia ya mtandao kupitia kiunganishi cha ajira.tamisemi.go.tz -

2.0 Sifa za Waombaji ni kama ifuatavyo:-

2.1 DAKTARI DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Udaktari wa Binadamu kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza Mafunzo ya Kazi “Internship” ya muda usiopungua mwaka mmoja na kupata Usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

2.2 DAKTARI WA MENO DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Udaktari wa Binadamu kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza Mafunzo ya Kazi “Internship” ya muda usiopungua mwaka mmoja na kupata Usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

2.3 TABIBU DARAJA LA II

Waombaji wawe na Stashahada ya Utabibu (Diploma in Clinical Medicine) ya muda wa miaka mitatu kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

2.4 TABIBU MSAIDIZI

Waombaji wawe wamehitimu Astashahada ya miaka miwili ya Tabibu Wasaidizi (Clinical Assistants Certificate) kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

2.5 TABIBU WA MENO DARAJA LA II

Waombaji wawe na Stashahada ya Tabibu Meno (Diploma in Clinical Dentistry) ya muda wa miaka mitatu kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

2.6 TABIBU MENO MSAIDIZI

Waombaji wawe wamehitimu Astashahada ya miaka miwili ya Tabibu Wasaidizi (Clinical Assistants Certificate) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

2.7 MFAMASIA DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Famasi kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliohitimu Mafunzo kwa Vitendo (Internship) ya mwaka mmoja na ambao wamesajiliwa na Baraza la Famasi (Pharmacy Council).

2.8 MTEKNOLOJIA (DAWA) DARAJA II

Waombaji wawe na Stashahada katika fani ya Uteknolojia wa Dawa (Diploma in Pharmaceutical Technology) kwa muda wa miaka mitatu kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Famasi (Pharmacy Council).

2.9 MTEKNOLOJIA MSAIDIZI (DAWA)

Waombaji wawe na Astashahada katika fani ya Uteknolojia wa Dawa ya Afya (Certificate in Pharmaceutical Technology) kwa muda wa miaka miwili kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Famasi (Pharmacy Council).

2.10 MTEKNOLOJIA (MAABARA) DARAJA II

Waombaji wawe na Stashahada katika fani ya Uteknolojia wa Maabara ya Afya (Diploma in Health Laboratory Sciences) kwa muda wa miaka mitatu kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya (Health Laboratory Practitioners' Council).

2.11 MTEKNOLOJIA MSAIDIZI (MAABARA)

Waombaji wawe na Astashahada katika fani ya Uteknolojia wa Maabara ya Afya (Certificate in Health Laboratory Sciences) kwa muda wa miaka miwili kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya (Health Laboratory Practitioners' Council).

2.12 MTEKNOLOJIA (MIONZI) DARAJA II

Waombaji wawe na Stashahada katika fani ya Mionzi (Diploma in Radiology/Radiography) kwa muda wa miaka mitatu kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Mionzi Tanzania (The Medical Radiology and Imaging Professionals Council).

2.13 MTEKNOLOJIA (MACHO) DARAJA II

Waombaji wawe na Stashahada katika fani ya Uteknolojia wa Macho kwa muda wa miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Baraza lao.

2.14 AFISA MUUGUZI DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Uuguzi kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali, waliohitimu Mafunzo kwa Vitendo (Internship) ya mwaka mmoja ambao wamesajiliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (Tanzania Nurses and Midwifery Council).

2.15 AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II

Waombaji wawe na Stashahada ya Uuguzi, ya muda usiopungua miaka miwili kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (Tanzania Nurse and Midwifery Council).

2.16 MUUGUZI DARAJA LA II

Waombaji wawe na Cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (Tanzania Nurses and Midwifery Council).

2.17 MTOA TIBA KWA VITENDO DARAJA LA II

Waombaji wawe na Stashahada ya miaka mitatu katika fani ya Fiziotherapia/ Mtoa tiba kwa Vitendo kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

2.18 AFISA AFYA MAZINGIRA DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Sayansi za Afya ya Mazingira (Bachelor Degree in Environmental Health Science) kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali pamoja na Mafunzo kwa Vitendo (Internship) ya mwaka mmoja ambao wamesajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira (The Environmental Health Practitioners Registration Council).

2.19 AFISA AFYA MAZINGIRA MSAIDIZI DARAJA LA II

Waombaji wawe na Stashahada ya Sayansi ya Afya ya Mazingira ya miaka mitatu kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira (The Environmental Health Practitioners Registration Council).

2.20 MSAIDIZI WA AFYA

Waombaji wawe wahitimu wa Kidato cha Nne waliofuzu Mafunzo ya Mwaka mmoja katika fani ya Afya, Afya Ngazi ya Jamii au mafunzo yoyote yanayofanana na hayo kutoka Vyuo vya Afya vinavyotambuliwa na Serikali.

2.21 KATIBU WA AFYA DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Uongozi wa Huduma za Afya (Health Services Administration) kutoka Vyuo Vikuu vinavyotambuliwa na Serikali.

2.22 AFISA USTAWI WA JAMII DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada au Stashahada ya Juu (Advanced Diploma) katika mojawapo ya fani zifuatazo: Social Work, Sociology, Psychology, Social Protection, Guidance and Counseling, Theology, Divinity, Child Protection, Social Policy, Any childhood development, Social Gerontology, au fani nyingine zinazofanana na Ustawi wa Jamii kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu vinavyotambuliwa na Serikali.

2.23 AFISA LISHE DARAJA LA II

Waombaji wawe na Shahada ya Kwanza ya Lishe, Sayansi Kimu na Lishe, au Sayansi ya Chakula na Teknolojia ya Chakula (BSc -

Nutrition, Home Economics and Nutrition, Food Science and Technology, Food Science) au Stashahada ya Juu ya Lishe (Higher Diploma in Nutrition) kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu vinavyotambuliwa na Serikali.

3.0 SIFA ZA WAOMBAJI KWA UJUMLA;

- i. Awe raia wa Tanzania;
- ii. Awe na umri usiozidi miaka 45;
- iii. Awe na namba ya kitambulisho cha Taifa;
- iv. Awe na vyeti kamili vya mafunzo ya fani aliyosomea;
- v. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au asiwe Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali; na
- vi. Asiwe mwajiriwa wa Serikalini au amewahi kuajiriwa Serikalini.

4.0 MAOMBI YOTE YAAMBATISHWE NA NYARAKA ZIFUATAZO:

- (i) Nakala ya Cheti cha Kidato cha Nne/Sita;
- (ii) Nakala za Vyeti vya Taaluma;
- (iii) Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa;
- (iv) Nakala ya Cheti cha Usajili kamili (*Full Registration*) au Leseni ya kufanya kazi ya taaluma husika; na
- (v) Maelezo Binafsi (CV), yakionesha umri, anuani kamili na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/namba za simu za kiganjani za wadhamini wasiopungua wawili.

5.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE

- (i) Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi katika Halmashauri watakazopangiwa;
- (ii) Waombaji wawe tayari kufanya kazi na Mashirika au Taasisi zilizoingia Ubia na Serikali;
- (iii) Waombaji waliosoma nje ya nchi wanatakiwa waambatishe *Equivalent Certificate* kutoka NECTA/NACTE/TCU; na
- (iv) Mara baada ya kupangiwa kituo cha kazi, hakutakuwa na nafasi ya kubadilishiwa kituo cha kazi.

- (v) Walimu wenye Ulemavu wenye sifa zilizoainishwa sawa na tangazo hili watume maombi yao ya kazi kwa nakala ngumu (hard copy) kwa Sanduku la Posta, rejista au EMS. Maombi yao yaeleze aina ya ulemavu wao na kuambatisha picha zao na yatumwe kwa anwani ifuatayo:

Katibu Mkuu,
Ofisi ya Waziri Mkuu,
S.L.P.980,
**40480 DODOMA (Aione: Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu
Wenye Ulemavu)**

Ili kupata maelezo ya kina kuhusiana na sifa za waombaji na taratibu za utumaji wa maombi kwa nafasi za Kada za Afya na Elimu, tafadhali bofya: **www.tamisemi.go.tz**

Maombi yoyote yatakayowasilishwa kwa njia ya posta au kuletwa moja kwa moja Ofisini hayatafanyiwa kazi isipokuwa kwa Walimu wenye ulemavu ambao maelekezo yao yametolewa katika kifungu cha 5(v). Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23 Mei, 2021 saa 5:59 usiku. Tangazo hili linapatikana katika tovuti ifuatayo: **www.tamisemi.go.tz**

Limetolewa na: Katibu Mkuu,
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,
Mji wa Serikali - Mtumba,
S.L.P 1923,
41185 DODOMA.